

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA SABA**

**KIKAO CHA KUMI NA SABA**

**4 MEI, 2017**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA SABA

**KIKAO CHA KUMI NA SABA – TAREHE 4 MEI, 2017**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**140. MHESHIMIWA KHATIB SAID HAJI (KONDE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

- (a) Je, bado kuna faida kwa Watanzania kuendelea kukimbiza Mwenge wa Uhuru kila mwaka, kama zipo ni faida gani;
- (b) Kama hakuna faida, Je ni lini Mwenge huo wa Uhuru utasitishwa.

## **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

### **141. MHESHIMIWA JORAM ISMAEL HONGOLI (LUPEMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Waathirika wa UKIMWI katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe wamekuwa wakipoteza maisha haraka zaidi kutokana na kutembea umbali mrefu kwenda kupata huduma za matibabu:-

Je, ni lini Serikali itaongeza bajeti ya ujenzi, vifaa tiba na madawa katika kila Kijiji na Vituo vya Afya kwa kila Kata.

### **142. MHESHIMIWA KEMIREMBE JULIUS LWOTA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa ni miongoni mwa Halmashauri mpya zilizoanzishwa mwaka 2015 na Watumishi wapatao 98 walihamishwa kutoka Halmashauri za Sengerema, Misungwi, Ilemela, Jiji la Mwanza, Kwimba na Magu lakini Watumishi hawa hadi sasa hawajalipwa fedha za uhamisho.

Je, ni lini Serikali itawalipa stahiki zao Watumishi hawa.

### **143. MHESHIMIWA ALLY SEIF UNGANDO (KIBITI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wananchi wa Kibiti wanaishukuru Serikali kwa kupata Mji Mdogo Kibiti na kufanya uchaguzi wa Mwenyekiti na Viongozi:-

- (a) Je, kuna tatizo gani hadi leo Mamlaka ya Mji haijaanza kazi na kumpata Meya;
- (b) Je, ni lini Serikali itapeleka Mkurugenzi wa Mji Mdogo.

### **WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

### **144. MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- TAGAMENDA SUBSTATION ni Kituo kikubwa kati ya vituo vinavyosafirisha umeme wa Gridi ya Taifa; kwani kinapokea umeme kutoka Mtera, Kidatu na Kihansi, lakini Vijiji vya Tagamenda, Ikuvilo na Wangama vinavyozunguka Kituo hicho havina huduma ya umeme ingawa ndivyo vinalinda Kituo hicho:-

- (a) Je, ni kwa nini Serikali inashindwa kutoa huduma ya umeme katika Vijiji vinavyozunguka Kituo hicho.

(b) Je, ni sababu gani zinazofanya Vijiji hivyo kukosa kupatiwa huduma hata ya Umeme wa REA.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.



*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
4 MEI, 2017**

**DKT. T. D. KASHILILAH  
KATIBU WA BUNGE**